Eneo la mafanikio kwa wanawake hasa mafanikio ya kiuchumi, imekuwa changamoto sana kwa siku za leo.

Wanawake wengi wamekuwa wakiamini ni ngumu kwa wao kufanikiwa, hasa wakikosa msaada wa mwanaume.

Ndio maana wengi wao wamekuwa wakitegemea huwenda mahusiano au ndoa itaweza kuwasaidia kutatua changamoto zao za kiuchumi, kitu ambacho hakina uhakika.

Wanawake wengi wamekuwa wakipitia nyakati nyingi ngumu na za machungu kwenye maisha yao, ambayo wakati mwingine imepelekea kutojiamini, kujidharau na mambo mengine mengi yasiyo furahisha juu yao.

Pamoja na changamoto hizo lakini kuna wanawake waliweza kuzikabiri na kuweza kupata mafanikio makubwa kwenye yale mambo walioamua kuyafanya.

Katika kitabu hiki cha mwanamke wa kazi nitakupa mwelekeo,mbinu na mikakati ya kukusaidia wewe kama mwanamke kufanikiwa

bila kumtegemea au kutegemea jitihada za mwanaume.

Katika kitabu hiki sifundishi kuwadharau, kuonyesha udhaifu, kupoteza utii kwa mwanaume wala kudharau nafasi ya mwanaume.

Ila lengo la kitabu hiki ni kukukwamua mwanamke ambaye bado maisha yako ya kiuchumi hayako sawa, na huwenda unawatoto ambao unawalea au wanakutegemea na hivyo wewe ni kama mhimili wa kutegemewa na wanao.

Au ni mwanamke ambaye unapitia changamoto za kiuchumi haijalishi umo kwenye ndoa au la. Lakini kitabu hiki ni kwa ajili yako.

Katika safari yangu ya kuwa mwalimu na mshauri wa mahusiano, nimekutana na changamoto nyingi sana za wanawake wakilalamika juu ya wanaume waliozaa nao kwamba hawawajibiki kutunza familia hasa watoto walio zaa nao.

Leo nimekuja na dawa hii ya kukufanya uweze kujitegemea kama mwanamke, na uweze kuwalea wanao kwa pesa yako mwenyewe, bila kumsumbua huyo mwanaume asiyeonyesha dalili yoyote ya kuwa upande wako wa kulea.

Ninaamini zaidi kwamba uchungu wa mtoto anayeujua ni mama zaidi, hivyo matatizo mengi ya watoto hutatuliwa sana na wakina mama.

Katika kitabu hiki nitakwenda kukupa mwanga juu ya safari uliyoamua kuianza ya kuwa mwanamke wa mafanikio.

Mbinu hizi zitakujengea ujasiri wa kusimama mwenyewe bila kumtegemea mtu na mwisho wa siku ukatoboa.

Karibu.